

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA WAZIRI MKUU**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TAARIFA KWA MAKATIBU TAWALA WA MIKOA NA WAKURUGENZI WA**  
**HALMASHAURI TANZANIA BARA KUHUSU UPIMAJI WA HALMASHAURI DHIDI YA**  
**MASHARTI YA KUPATIWA RUZUKU ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2011/12**

Ninapenda kuwaarifu Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara, Wakurugenzi wote wa Halmashauri Tanzania Bara na pia Umma kwa ujumla kuwa zoezi la Upimaji wa Halmashauri zote dhidi ya masharti ya kupatiwa Ruzuku ya Maendeleo na Vigezo vya Kiutendaji chini ya Mfumo wa Kuzipatia Halmashauri Ruzuku ya Maendeleo (LGDG System) kwa mwaka 2011/12 linatarajiwa kufanyika mwezi Februari 2011.

Ratiba kamili inayoonesha tarehe ya kufanyika kwa zoezi zima la upimaji mtapelekewa hapo itakapokuwa tayari.

Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wanaelekezwa kuhakikisha kuwa maandalizi yote kwa ajili ya upimaji yanakamilishwa vilivyo na kuhakikisha kuwa Menejimenti na Viongozi wa ngazi zote za Halmashauri na Wananchi kwa ujumla, wanayafahamu Masharti yanayopaswa kutimizwa, taarifa mbalimbali zinazotakiwa na vyanzo vyake, utaratibu wa Upimaji na Mpangilio wa Masharti yanayopaswa kutimizwa kwa ajili ya kupata Ruzuku. Upimaji huu utahusu pia masharti ya kupata fedha chini ya Programu za kisekta zilizojumuishwa kwenye Mfumo wa kuzipatia Halmashauri Ruzuku ya Maendeleo, zikiwemo zile za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Agricultural Sector Development Programme – ASDP), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Vijijini na Programu ya Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Mnajulishwa pia kwamba Mwongozo wa Upimaji utakaotumika ni wa Novemba, 2010. Mwongozo wa Upimaji uliotumika miaka miwili iliyopita umefanyiwa marekebisho katika baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na muundo wa timu ya upimaji, aina za ufaulu kwenye upimaji (Nzuri sana, Nzuri, Wastani na Dhaifu), maeneo ya kiutendaji yanayopimwa. Mwongozo uliorekebishwa umepelekwa kwenye kila Mkoa na Halmashauri kwa ajili ya kuutumia. Ieleweke ya kuwa Mwongozo huu haukubadilika sana ukilinganishwa na ule uliopita.

Zoezi hili la Upimaji litafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wataalam Washauri watakaopatikana kwa njia ya zabuni ya ushindani.

Kwa mara nyingine, mnakumbushwa kwamba ni muhimu Mikoa, Wilaya na Halmashauri zikaanza sasa kufanya tathmini ya ndani kwa kujipima wenyewe (Internal Assessment) kabla zoezi hili halijaanza. Ikiwa utahitaji ufafanuzi katika jambo lolote, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa katika OWM-TAMISEMI kwa kutumia simu na. 026 23 21599 au 022 27 00769.

**J. A. Sagini**  
**KAIMU KATIBU MKUU**  
**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA**  
**SERIKALI ZA MITAA**